# *HUKO KADESH BARNEA*

Aliogopa sana, moyo wake ulikuwa karibu unakwenda mbio maili tisini kwa saa, ilivyoonekana. Alikuwa nyumbani muda mfupi uliopita, naye alikuwa chumbani akijaribu kuuvumisha na kuuboresha.

2 Na, vema, inanikumbusha juu ya Ndugu Moore, wakati mvulana wake mdogo, alisema alitaka kuhubiri. Alikuwa na umri wa takriban miaka saba au minane, akaendelea kusema, "Baba, nataka kuhubiri." Kwa hiyo usiku mmoja, mbele ya kusanyiko, Bw. Moore alisema, "Sasa, jamani," kasema, "David, anayeketi hapa," ameketi pale juu kama kasisi wa siku nyingi, mwajua, na kichwa chake kimeinuliwa juu. Akasema, "Anataka kuhubiri kidogo, usiku wa leo." Kwa hiyo, akakimbia jukwaani. Akaruka chini kutoka kwenye kiti chake, akakimbilia kule, mwajua, akasimama. Naye alifikiri angeyaingilia moja kwa moja. Ndipo akatazama upande mmoja, na mwingine, kasema, "Kweli haiwezekani," akarudi na kuketi chini.

3 Nimeona mara nyingi, nilidhani haitawezekana. Lakini tu . . . Hiyo ilikuwa ni sawa, hata hivyo.

4 Mama zao walikuwa wakituimbia, Mabel na Meda. Mngependa kuwasikia wakiimba tena wakati mmoja, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ningependa tu kuwasikia wakiimba. Labda tuwafanye waungane Jumapili ijayo usiku, na kuniimbia wimbo walioimba nilipoondoka kanisani. Mnakumbuka wakati, u—ulikuwa ni upi?

> Mchanga umefagiliwa katika nyayo za miguu
> Mgeni . . .

Na kisha:

> Watakuja kutoka Mashariki na Magharibi, (Hebu tuone.)
> Kula pamoja na Mfalme, kula kama mgeni Wake.

5 Nafikiri ndivyo unavyoenenda. Ningependa kuwasikia. Ni wangapi wangependa kuwasikia, yapata Jumapili ijayo usiku, kama tuko hapa? Mngependa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, hakika. Mabel, uko hapa? Je, yuko hapa, Doc? Anasikia, na Meda yuko kule nyuma, basi wanaweza kujizoeza kidogo. Maana, wasichana watawakimbia, baada ya kitambo kidogo, sivyo? Hiyo ni kweli. Inawabidi kufanya mazoezi kidogo sasa, na waanze juma hili lijalo.

6 Usiku wa leo, nikishuka, na dakika chache tu zilizopita, familia ilikuwa imeondoka, nami nilikuwa peke yangu na Bwana, kuomba kidogo. Niliteremka kwa gari nikapita maskani

ya kale nikaona magari yakiwa yamepangwa hapa nje. Mnajua, inarudisha kumbukumbu za kale, za muda mrefu uliopita, wakati tulipokuwa na, humu ndani, tulipoingia, tukawa na ibada nzuri sana, zilizoendelea hadi saa nane na saa tisa usiku. Watu waliketi tu pande zote, pamoja.

7 Mnajua, wengi wa hao wazee wa kale wako hapa kaburini leo. Ninamaanisha mwili wao, lakini wao wako Utukufuni. Na vizazi vinaendelea kuja, vile vichanga vikifuatilia. Haitachukua muda mrefu hadi tutakuwa tumeondoka. Hicho kizazi kingine kitaninii . . . hicho kingine, vijana, watachukua nafasi yetu. Kwa hiyo inatupasa kuishi kila siku, sivyo, kwa ajili ya Bwana tu, Yeye pekee.

8 Sasa, najua kesho ni siku ya kazi kwa watu ambao inawabidi kutoka na kwenda kazini. Kwa hivyo sisi . . . tutajaribu kutoka mapema usiku wa leo. Je, ibada ya ubatizo, kuna chochote kitakachoifuata hii? Vema.

9 Sasa, Biblia hii ya kale iliyobarikiwa ndiyo ramani ya kuelekeza . . . tangu utotoni hadi—hadi kaburini, na hadi Mbinguni, kote kote. Nasi tunaipenda, kwa sababu Humu ndani ndimo tunamopata mpango wa wokovu wa kuokoa kabisa.

10 Sasa, kabla hatujaifungua, hebu na tuzungumze na Mwandishi, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi.

11 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe, usiku wa leo, kwa yote ambayo yamefanywa, tayari katika ibada, kwa nyimbo na kwa ajili ya . . . yote ambayo tayari yamefanyika. Nasi tunashukuru usiku wa leo kukusanyika hapa chini ya paa la jengo hili dogo, katika Jina la Bwana Yesu, pamoja na ahadi hii ya neema, kwamba, "Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao." Nasi tunajua ya kwamba Wewe uko hapa.

12 Nasi tuna furaha sana kujua, ya kwamba, baada ya miaka elfu moja na mia tisa ya kuhubiri Injili, na—na historia ya ulimwengu ikiendelea, hata hivyo Wewe unabaki vile vile. Mabadiliko ya wakati, mabadiliko ya watu, mabadiliko ya taifa, mabadiliko ya shauku, na misimamo, lakini Wewe unabaki vile vile. Nasi tunafurahia sana hilo, usiku wa leo, Baba.

13 Kwa maana, tuna furaha ya kwamba tunaweza kusoma Neno Lako, na kuona kile Wewe ulichokuwa wakati huo, na kujua kwamba tunamkaribia Baba yule yule mwenye upendo, anayesamehe na anayeelewa ambaye wakati mmoja alitembea kwenye fuo za pwani ya Galilaya; akasulubiwa, akichukua mahali petu, na akawa mwenye dhambi aliyekufa msalabani, badala yetu, kujitwika Mwenyewe dhambi zetu, kuziondolea mbali, na akatupwa kuzimuni. Naye nabii alikuwa amesema, "Sitaiacha nafsi yake kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu." Ndipo siku ya tatu akafufuka tena, akapaa Juu, ambapo umeketi usiku wa leo katika mkono

wa kuume wa Ukuu wa Mungu, kufanya maombezi juu ya maungamo yetu. Nasi tuna haki na majaliwa ya kukiri kwamba, mali yetu binafsi ambayo imenunuliwa kwa Damu Yako, chochote ambacho ulijumuisha katika mpango Wako wa ukombozi ulipokufa na kufanya upatanisho pale Kalvari.

14 Na, usiku wa leo, Baba, tunaomba baraka maalum kwa kila msafiri ambao wamekusanyika chini ya paa hapa, usiku wa leo, maskanini.

15 Tunaomba, pia, Baba, kwa ajili ya wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, walio nje ya safina, usiku wa leo, wasiokujua Wewe. Tunaomba ya kwamba utakuwa pamoja nao, na kuwavuta Kwako, usiku wa leo, na Roho Mtakatifu abishe hasa mioyoni mwao, na kuwavuta kwa Mungu Baba yetu. Tujalie, Bwana.

16 Bariki kila kanisa na kila mkutano unaoendelea ulimwenguni kote, leo na usiku wa leo. Na wahudumu wote wavuviwe kuhubiri, na mioyo ya watu na sikio yatahiriwe, ili kusikia na kuelewa, naye Mungu atapokea utukufu. kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

17 Basi Bwana na aongeze baraka Zake usiku wa leo, tunapokuja msalabani, kufundisha kidogo juu ya Neno. Hili ni kama somo la shule ya Jumapili.

18 Mnajua, nilikuwa nikiwazia, muda mfupi uliopita, nikiketi pale juu. Mwajua, lingekuwa jambo zuri sana wakati mwingine, kama. . .Kuna jengo kubwa tupu, mjini hapa chini, jumba la kale la michezo ya kuigiza la Ndoto. Nakisia litaenea watu elfu moja mia tano hadi elfu mbili. Nalo lingekuwa zuri sana, kama tungeweza kulipata, siku moja, au labda mwendeleo wa Jumapili kadhaa mfululizo, yapata majuma matano, na tufanye ibada ya uponyaji Jumapili alasiri, katika jumba la kale la michezo ya kuigiza la Ndoto hapa chini, na kutangaza ibada kwenye mojawapo ya vituo vya mahali hapa, kwa saa moja. Haigharimu pesa nyingi sana; takriban dola kumi na tisa, ishirini, kitu kama hicho, kwa saa moja. Nitafurahi kulilipia, mimi mwenyewe, na kama mikutano yangu huko nje itaifadhili. Kwa ajili tu ya watu hapa kuletwa, na mahali pazuri pa kuwapeleka, kwa ajili ya waongofu.

19 Na, mwajua, na kwa hiyo nilifurahia sana ujumbe wa mchungaji wetu asubuhi ya leo, kuhusu "kuvua." Nami najua ninyi nyote mliufurahia. Na hiyo ni kweli. Na—nasi hatuna budi kuwaingiza samaki kwenye wavu, kama alivyosema. Na hiyo ni kweli, mnaona, hamna budi kuwaingiza samaki kwenye wavu. Na kisha, pamoja, mbona, tunasimama.

20 Sasa, mimi, jana jioni, kwa Ndugu Junior Cash, naamini ndilo jina lake. Tulikuwa kule kuzungumza kwa niaba yake, jana jioni, naye Bwana akashuka kwa njia ya ajabu. Nao wakamleta msichana. Kitu pekee nilichoona, ambacho kingeweza kuwa

cha kawaida, ambacho ungeliweza kuona kwa jicho lako, kilichokuwa jukwaani, kilikuwa ni msichana mweusi kutoka sehemu za chini za Indiana, chini ya New Albany ama popote pale, alikuwa amepata ajali, naye alikuwa amekata mishipa katika sikio pamoja na sauti, hata asingeweza kuzungumza wala kusikia. Nao mshipa ulikuwa umebanwa mahali fulani, ambao ulipoozesha ubavu wake. Basi huyo msichana, mama yake, huku akiwa na magango makubwa, wakijaribu kumwelekeza kule. Msichana mdogo tu, msichana, na labda umri wa miaka kumi na sita, kitu kama hicho. Na kwa namna fulani au nyingine, Roho Mtakatifu alionekana tu kuiweka Afrika papo hapo mbele yangu. Nami nikaitazama.

21 Nami nina ono lililoandikwa papa hapa katika kitabu, kwamba marejeo ya Afrika yatakuwa makubwa kuliko mkutano wa kwanza wa Afrika.

22 Ndipo basi, bila watu kujua kilichokuwa kikiendelea, bali ono likitukia. Ndipo nikasema, "Baba wa Mbinguni . . ."

23 Sio kwamba tunaomba miujiza. Biblia ilisema, "Kizazi dhaifu na cha zinaa hutafuta miujiza." Nasi hatutafuti miujiza, lakini Mungu hufanya miujiza. Wakati uo huo Yeye alisema ya kwamba, alikuwa akifanya miujiza. Lakini—lakini tukiitafuta, hatuna budi kuwa na miujiza, kitu cha kutuonyesha, ushahidi fulani kwamba—kwamba tumeokoka, au kitu kama hicho; siamini katika ushahidi. Ninaamini ushahidi kwamba tumeokolewa, tuliliamini Neno la Mungu. Hilo ndilo jambo bora zaidi nilijualo. Ndipo matunda yanafuata.

24 Sasa, nilimwuliza kama angelijalia tu, kama—kama ishara kwamba ulikuwa ni wakati wa kurudi Afrika; ambayo, mawasiliano yetu yanazidi kuimarika kila wakati. Basi tulipomwombea msichana huyo, angeweza kuongea na kusikia na kusogea. Ilikuwa ni ajabu tu kuona kile ambacho Bwana wetu angeweza kufanya.

25 Na kwa hiyo tuna furaha usiku wa leo kwa ajili ya hilo, tunajua ya kwamba makazi hayo mazuri, popote yalipo, tuna furaha sana usiku wa leo kumwona msichana huyo. Ilifanyikaje, wakati mishipa yote ilikatwa kutoka kwake? Mnaona? Hamna njia, hata kidogo. La, hamna kitu. Ilikuwa tayari imekatwa na kubanwa, mishipa ya ulimi au sauti, na ya kusikia. Ambayo, yote miwili iko kwenye mshipa ule ule, lakini ilikatwa na hiyo ajali. Lakini, Mungu, kwa namna fulani . . .

26 Ni wangapi walikuwepo na kumsikia huyo msichana akizungumza? Hebu tuone hapa. Hiyo ni kweli. Naye angeweza kuzungumza na kusikia na kuongea.

Ningezungumza *hivi*. Nikasema, "Unanisikia?"

Akasema, "Ndiyo."

"Unanisikia tena?" Nikasema, "Sema,'Mama.'"

Akasema, “Mama.”

Nikasema, “Sema, ‘Yesu.’”

Akasema, “Yesu,” na kuendelea mbele na kuongea.

27 Kwa hivyo, Bwana ni wa ajabu, sivyo? Mwingi wa rehema.

28 Na halafu nikiwa huko nje kutoka kwenye ibada za uponyaji sasa kwa majuma mawili, kidogo ilifanya moyo wangu kudunda kwa nguvu tena, kujiandaa kwa ajili ya ibada nyingine.

29 Sasa, katika Kitabu cha Hesabu. Ninapenda Agano la Kale. Nasi tutakuwa na somo usiku wa leo, sasa juu ya Kitabu cha Hesabu. Hesabu, mlango wa 13 na kifungu cha 30, tusome tu kifungu kimoja kwa ajili ya msingi, na kwa mwanzo.

30 Na halafu, mnaona, kama tukisoma kifungu kimoja kutoka katika Biblia. . .Ninajua jambo hili moja: neno langu litashindwa, kwa sababu mimi ni mwanadamu. Lakini Neno hilo la Mungu halitashindwa kamwe, kwa sababu ni Neno la Mungu. Na, kwa hiyo, kifungu kimoja kutoka Hapa kitatoa msingi wa kutosha hata kila mtu ajaye atabarikiwa, kwa sababu si zaidi tu ya kusoma Neno.

Sasa, katika kifungu cha 30:

> *Kalebu akawatuliza watu mbele ya Musa, akasema, Na tupande mara, tukaitamalaki; maana sisi. . . tunaweza kushinda.*

31 Basi Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno. Sasa, somo langu usiku wa leo ni: *Huko Kadesh-Barnea*. Na somo hili ambalo tunalizingatia, kwa msingi mdogo tu, kulileta hadi mahali ambapo, Bwana akipenda. . .

32 Haya yote, bila shaka, hayakupangwa awali. Yanasemwa tu kwa uvuvio, jinsi tu yanavyotolewa. Sikuwahi kupata mafunzo ya kujifunza jinsi ya kulihubiri. Nami nimeijaribu, mara nne ama tano, na kuyavuruga yote kabisa. Si—sijui jinsi ya kulifanya. Lakini, kweli ninampenda, na ninamtegemea Yeye. Nami najua ninyi nyote mnamtegemea, pia.

33 Kwa hiyo, sasa, hapo mwanzo, hii ni picha, ambayo Mungu. . .Mchezo mkubwa wa kuigiza wa Biblia, ambao Mungu ameweka taratibu hapa kwa ajili yetu, ili kwa huu tupate kufanikiwa. Ninaamini, huko katika Waebrania mlango wa 10, ama mlango wa 12, ilisema, “Kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi, tupate kupiga mbio kwa subira mashindano yaliyo mbele yetu, tukimtazamia mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu, Bwana Yesu Kristo.”

34 Sasa, Agano lote la Kale, na wahusika Wake wote na tabia zao, walikuwa tu ni kivuli tangulizi cha—cha kabari, au jiwe la msingi, Agano Jipya, kilichounganisha torati na kipindi hiki cha

wakati pamoja. Watu wengi wametaja hiki kama kipindi cha wakati wa Ukristo, lakini sivyo. Hiki ni kipindi cha wakati wa Roho Mtakatifu. Kipindi cha Ukristo kilidumu miaka mitatu na miezi sita. Torati ilidumu miaka mia kadhaa. Halafu basi kipindi cha wakati wa Ukristo ndicho kilishikamanisha, ama kuunganisha, Agano Jipya na la Kale pamoja.

35 Na mara nyingi, katika Biblia, tunaona, na mara nyingi tunarejea kwenye, "Matendo ya Mitume," kinavyoitwa. Sikuzote napenda kukitaja kama "Matendo ya Roho Mtakatifu ndani ya Mitume." Kwa sababu, mitume walikuwa ni wanadamu tu, bali ilikuwa ni Roho Mtakatifu ndani ya mitume, akileta huduma Yake. Naye Roho Mtakatifu ni Roho wa Bwana Yesu Kristo aliyelishukia Kanisa, kuendeleza kazi za Bwana Yesu, katika kuondoka Kwake. Ni kutoa Nuru ya Injili, kwa nuru ndogo zaidi, kuliko ilivyokuwa wakati Kristo alipokuwa hapa.

36 Kama mwezi na jua. Mwezi hujitokeza, kutoa mwanga wakati jua halipo, mpaka linapoweza kuchomoza tena, ndipo mwezi unatoweka. Na jua ni nuru angavu zaidi, hata huzima mwanga wa mwezi. Lakini mwanga wa mwezi ni nini? Ni uakisi wa jua kwenye mwezi.

37 Na hiyo ni kama Kristo. Alipokuwa hapa, Yeye alikuwa Nuru ya ulimwengu. Akaenda zake, na kuliangazia Kanisa Lake tena, lipate kuiakisi Nuru Yake ulimwenguni leo hii, tupate Nuru ya kutembelea mpaka atakaporudi. Ndipo basi yote-kwa-yote atapewa Yeye. Naye ataketi kwenye kiti cha enzi cha Mfalme Daudi, na kutawala milele na milele.

38 Sasa, Agano la Kale likiwa ni mfano mzuri sana, tunafananisha pale na kuona mambo hayo yote yaliyowapata hao watu, tupate kuangalia mifano.

39 Sasa, Mungu akiwa mwenye enzi, na kama vile nilivyokuwa tu nikifundisha leo, katika nyumba ambayo nilialikwa nije kwa chakula cha kutwa. Walitaka kujua kama wangewajua wapendwa wao, wakikutana nao huko Utukufuni.

40 "Vema," nikasema, "bila shaka, tutawajua." Mnaona, tu—tuko katika ninii . . .

41 Tuna miili mitatu mbalimbali tunayoishi. Mmoja ni wa kibinadamu, huo mwingine ni wa mbinguni, na mwingine ni ule uliotukuzwa. Na basi kama tunafahamiana katika mwili wa mwanadamu, mwili unaopatikana na mauti, ni zaidi sana vipi tutafahamiana, mmoja kwa mwingine, katika mwili wa utukufu!

42 Ni kama vile, kama torati ingeweza kutoa kitu kizuri, ni zaidi sana vipi neema inaweza kutoa kitu kikubwa zaidi, kwa sababu ni kuu kuliko torati!

43 Na ikiwa mwezi unaweza kutoa sehemu fulani ya mwanga, ni zaidi sana vipi jua litaangaza zaidi, linapochomoza! Nasi bila shaka tutafahamiana.

44 Na sasa ni kama tu, kama ninavyosema, tunaendelea kukua katika maarifa, mwanadamu. Unajua zaidi sasa kuliko ulivyojua ulipokuwa mvulana au msichana mdogo, kwa sababu unapata hekima zaidi. Na jamii nzima ya wanadamu inapata hekima zaidi. Lakini, je, mliona, ulimwengu wa wanyama haupati hekima zaidi? Unajua, unaishi katika makazi bora sasa kuliko babu yako alivyoishi. Na pengine watoto wako wataishi katika makazi bora zaidi kuliko uliyo nayo sasa.

45 Lakini hivi majuzi tu, ninaamini, katika *Reader's Digest* ama mahali fulani, nilikuwa nikisoma makala ambapo walichukua ndege mdogo, na kumweka kwenye kizimba, bila kitu cha kujengea kiota. Ndipo ikambidi kutaga mayai yake kwenye sakafu ya hicho kizimba. Nao wakaangua, makinda wa ndege. Nao wakawachukua hao makinda na kuwaweka kizimbani, bila kitu chochote cha kujengea kiota. Walipowaangua, hadi vizazi kumi na vitano, vizazi kumi na vitano mbalimbali, kuona kama ingebadilisha maumbile. Basi, hiyo ingechukua miaka kumi na mitano, kwa sababu hao ndege wana kiota kimoja tu cha mayai kwa mwaka. Ndipo baada ya miaka kumi na mitano, wakawafungulia wale vifaranga wengine, mahalifa wake, wa—wa miaka kumi na mitano, hajawahi kuwa na majani ya kujenga kiota, wala chochote kile; kisha wakamweka huyu ndege mahali fulani, na jambo la kwanza alilofanya lilikuwa ni kuondoka na kujenga kiota. Ndege wanajenga kiota chao kama tu walivyofanya katika bustani ya Edeni.

46 Lakini mwanadamu anaendelea kusonga mbele, anaendelea kupata hekima zaidi. Wote. . .Babu yako, kama nilivyosema, alikwenda kumwona nyanya, kwenye mkokoteni wa maksai. Baba yako aliendа kumwona mama, akiendesha farasi na kigari chake. Nilikwenda kumwona mke wangu, katika gari la Ford muundo wa T. Mvulana wangu ana la silinda nane liendalo kasi, vyovyote mnavyoliita. Pengine wajukuu wangu watakuwa na ndege.

47 Hiyo ndiyo njia, tunaendelea kupiga hatua, kwa sababu tunayo nafsi. Sasa, ndege hana nafsi. Lakini sisi tunayo nafsi. Sisi si muumbaji; lakini tunaweza kupotosha. Sasa, hatuwezi kuumba mbao; lakini tunaweza kuchukua mbao, Mungu akisha kuziumba, na kujenga nyumba kwazo. Kwa sababu, sisi ni watoto wa Mungu, wana na binti za Mungu. Haijalishi tumeanguka jinsi gani, bado inatupasa kutambua kwamba sisi ni wana na binti za Mungu. Katika hali yetu ya kuanguka, tungali ni wana na binti.

48 Mungu hutoa ahadi; Mungu hana budi kutimiza ahadi hiyo. Loo, natumaini mnaliona. Laiti mngaliweza kuelewa, enyi kanisa, usiku wa leo, na kutambua, msingekuwa mkitangatanga huku na huko, na kujiunga na kanisa *hili* na kanisa *lile*. Hamngekuwa mkiyatafuta mambo ya ulimwengu, kujiburudishia. Hamngekuwa mkitangatanga kutoka ibada

moja ya uponyaji hadi nyingine. Mngeliamini Neno la Mungu, na kujua ya kwamba yamekwisha. Bila shaka. Mungu anapotoa ahadi, hawezi kuondoka kwenye ahadi hiyo. Yeye—Yeye anawajibika kulitimiza Neno Lake.

49 Nilimsikia mtu akisema, "Vema, wao—wangerudi nyuma, na kurudi." Nawe ungeweza kufanya hivyo. "Naam, nimepotea pamoja na Mungu." Kama uliwahi kupatikana Naye, hutawahi kupotea pamoja Naye, kwa sababu Mungu hawezi kukuokoa halafu akupe kisogo na kukuondolea mbali. Kama angefanya hivyo, angeshinda kusudi Lake Mwenyewe. Kwa hiyo, Yeye hawezi kufanya hivyo. Kwa hiyo wakati Mungu . . .

50 Tunapata hekima zaidi, lakini Mungu alikuwa asiye na kikomo kwanza kabisa. Alikuwa mkamilifu. Hapati hekima zaidi. Yeye ni yeye yule daima. Kwa hiyo, kama janga fulani likitokea, naye Mungu akatenda *hivi-na-hivi* kwenye janga hilo; basi kama janga hilo likitokea tena, kama Yeye hatendi vivyo hivyo, Yeye alikosea alipotenda *hapa*. Mnaona? Kwa hiyo hana budi kuwa yeye yule, wakati wote, bila kujali wakati wowote.

51 Na jinsi watu wanavyoweza kueleza na kujaribu kuondoa Nguvu za Uungu, siwezi kuelewa. Kwa sababu, ikiwa Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Nguvu Zake ni zile zile, mtazamo Wake ni ule ule. Na kama tu alivyokuwa wakati huo, ndivyo alivyo sasa, na atakuwa hivyo milele. Haiwezekani kabisa kuondoa chochote kutoka Kwake. Hamna lingine.

52 Na kama Yeye aliinuka katika siku za safari Yake duniani, na kuwaponya wagonjwa ambao madaktari hawangeweza, akawaponya; kama alitenda hivyo katika janga hilo, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, hana budi kutenda vivyo hivyo leo, la sivyo aliwakosea hao watu. Mnaona?

53 Kama Yeye alitoa ahadi pale, na ikabidi adumu nayo, akitoa ahadi *hapa*, hana budi kudumu nayo. Hana budi kudumu nayo. Mungu hana kasoro yoyote, wala na ahadi Yake. Kosa liko ndani yetu, hakuna imani ya kuliamini, ama kumshikilia katika Neno Lake.

54 Sasa, mnaona, kama tungekuwa na akili ya ndege, tungetenda kama walivyofanya hapo mwanzo.

55 Lakini, tunakuwa werevu sana, tunauelezea vingine kabisa, na kusema, "Loo, hicho kilikuwa ni cha wakati uliopita," nasi tunajenga hali nyingine tofauti. Badala ya kuliamini Neno la Mungu, tunaanzisha tu shirika jipya. Mnaona? "Vema, *hivi* ndivyo Mungu atakavyofanya, na *hivyo* ndivyo Mungu atakavyofanya."

56 Iwapo sisi, kama tu ndege, wala hatukubadilika, wala hatukuwa na uhuru wa kujichagulia, tungeliamini tu Neno la Mungu, na hilo lingetosha, na ni hivyo tu. "Mungu alisema hivyo, kwa hiyo hakuna lingine." Inapendeza jinsi gani, kuona kwamba

Mungu wa kweli na aliye hai angali anaishi leo. Katikati ya machafuko yote, Mungu angali hai na anatawala.

57 Sasa, watu hawa wa agano, Israeli, huko—huko chini Misri, kwa sababu ya maasi, na kumwuza ndugu yao Yusufu. Nao walipelekwa huko chini Misri, na wakakaa huko miaka mia nne, chini ya utumwa. Nataka muone, kamwe hawakupoteza agano lao. Walipoteza uhuru wao, sio agano lao. Mungu alipofanya agano na Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, kwamba aliapa kwa nafsi Yake kwamba angemwokoa Ibrahimu na uzao wake baada yake, Mungu anawajibika kutimiza ahadi hiyo.

58 Naye amewajibika tu kwako, juu ya ahadi hiyo, kadiri alivyokuwa kwa Ibrahimu, juu ya hiyo ahadi. Hiyo ni kweli, kama wewe ni Uzao wa Ibrahimu. Unakuwaje uzao wa Ibrahimu? "Sisi tuliokufa katika Kristo tunachukua Uzao wa Ibrahimu," Biblia inasema, "na tu warithi sawasawa na ile ahadi," basi Mungu anawajibika kwako kadiri alivyokuwa kwa Ibrahimu. Aisee, hiyo ingeondoa woga wote kwake! Mungu hataki uogope chochote. Tulia kwa uchaji juu ya yale Yeye aliyosema.

59 Tunachohitaji siku hizi ni mtu fulani ambaye atayapa changamoto majira tunayoishi. Hiyo ni kweli. Katika siku ambapo hitilafu na kila kitu kingine kimenyemelea ndani, chini ya jina la dini na kadhalika, na chini ya jina la wokovu, Injili. Tunahitaji mtu fulani kuinuliwa kati yetu, kama vile Mungu alivyomwinua Musa kuchukua mahali hapo katika siku hiyo. Naam.

60 Hawakuwa wamepoteza agano lao. Walikuwa wamepoteza uhuru wao. Walikuwa watumwa, lakini agano lingali lilidumu.

61 Na siku moja kule chini, walipokuwa wakiugua na kulia, chini ya wanyapara wa Misri, kwa sababu walikuwa watumwa. Nawatakeni muone picha hii nzuri. Na hii ingekuwa nzuri kwa washika sheria. Sikilizeni. Mungu kamwe hakushuka na kusema, "Sasa, kama utafanya jambo *fulani*. Ikiwa utafanya jambo *fulani*." Neema ya Mungu ilitoa mwokozi, Musa. Hiyo ni kweli. Musa hakuletwa chini ya masharti yoyote, bali kwa neema kuu, Mungu alimtuma Musa. Sio tu mwokozi, bali neema ilitoa mkombozi; bila sheria yoyote, bila chochote. Neema kuu tu ya Mungu, alimtuma Musa kuwa m—mkombozi na mwokozi wa taifa, kuwatoa.

62 Ninapowazia hilo, ndipo ninaanza kukumbuka kwamba Mungu yeye yule, aliyekuwa pamoja na watu wa agano kule Misri, hakika ni . . . Chini ya dhiki na kutojali ambako kanisa liko usiku wa leo, Yeye, kwa neema ya Utu Wake mwenyewe, atatuma mkombozi. Tuna hakika tu ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, katika siku hizi za mwisho, kadiri tunavyoketi katika kanisa hili usiku wa leo. Mungu ametenda kwa watu wa agano, bila juhudi yoyote yao. Lakini, Yeye alituma bure kutoka

Mbinguni, kwa watu Wake wa agano, tendo la neema. Juu ya ukuu wa ahadi Yake, alimtuma Musa.

63 Na katika matatizo yale yale, wakati watu walipokuwa utumwani, na chini ya kila kitu, nira ya dhambi, na magonjwa na shida leo hii; Yeye ana uhakika wa kumtuma Yesu Kristo mara ya pili, kama alivyomtuma Musa mara ya kwanza. Matatizo yalipotokea, Mungu alitenda kwa neema kuu. Yeye hana budi kufanya jambo lile lile chini ya tendo lile lile, la sivyo alikosea alipotenda kule nyuma. Mnaliona?

64 Ninachojaribu kufikia ni hiki. Dhambi kuu kuliko zote ninayoipata Kanisani siku hizi ni kutokuamini. Hiyo ndiyo dhambi pekee iliyopo. Hakuna dhambi nyingine ila kutokuamini. Ni kiasi gani cha hiyo ni usiku huko nje, giza ni kiasi gani? Usingeweza kusema, "Kiasi *hiki* ni giza," wakati kutoka mikononi mwangu ni giza tupu.

65 Sasa kuna njia moja tu ya kung'amua na kuitambua dhambi. Hiyo si kwa kama unakunywa pombe, au kama unavuta sigara, au kama unacheza kamari. Inang'amuliwa *hivi*: kwa sababu wewe ni asiyeamini, ndio unafanya hivyo. Na hiyo ni kweli. Ati kwa sababu unacheza kamari, kwa sababu unasema uongo, kwa sababu unaiba, mambo hayo si dhambi. Hayo ni matokeo ya dhambi. Hiyo ni kwa sababu ndani yako inakaa roho tofauti. Kama ungalikuwa mwaminio, mwaminio thabiti, mambo hayo yangekuwa yamekufa na giza kama vile usiku ulivyo mbele yako. Bila shaka. Mnaona? Mambo hayo ni matokeo ya kutokuamini.

66 Katika Yohana Mtakatifu mlango wa 3, Yesu alisema, ya kwamba, "Asiyeamini amekwisha kuhukumiwa." Hata huufikii msingi wa kwanza. Umehukumiwa, kwanza kabisa.

67 Kwa hivyo, haimaanishi kwamba unapaswa kuwa na kijiti cha kupimia kanisani mwako, "Ukifanya *hivi;* ukizingatia kanuni *hizi*; ukizingatia kanuni *hiyo*." Mara nyingi, watu wataweka kando vitu vidogo kama hivyo, wapate kuwa wafuasi wa kanisa; na jambo hilo lingali moyoni mwao, nao wanateleza na kulifanya. Lakini wakati mtu ametimiza matakwa ya Mungu, na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, mambo hayo yanaondolewa maishani mwake. Hataki kuyafanya.

68 Je, ungeweza kumwazia nguruwe? Nguruwe atakwenda kwenye lundo la samadi, naye atakula. Si—simlaumu. Yeye ni nguruwe. Hilo ndilo linalomfanya afanye hivyo. Lakini hutawahi kumfanya mwana-kondoo atende hivyo. Kwa sababu, kuna asili mbili. Nguruwe ana asili moja, na mwana-kondoo ana asili nyingine. Na maadamu unaweza kuweka asili iyo hiyo katika nguruwe huyo, haijalishi unajaribu kumsafisha kiasi gani, atakuwa asili ile ile kwa sababu yeye ni nguruwe, kwanza kabisa.

69 Na kwa hiyo, mara nyingi, tunawachukua watu na kuwaleta kanisani, na kadhalika namna hiyo, kuwafanya washiriki, wakati hawajaokoka kamwe.

70 Hiyo ndiyo sababu siku hizi, kuna kuchanganyikiwa jinsi hii, kama kulivyo mbele za watu, hawajui waelekee upande gani. Wanaona watu wakikiri Ukristo, wala hawana tofauti na ulimwengu. Ni kwa sababu huyo mtu hajawahi kukutana, au kuzaliwa mara ya pili, kamwe hajamkubali Bwana Yesu, kamwe hajamwamini. Huenda wamesisimkwa. Huenda walicheza. Huenda walipaza sauti. Huenda walinena kwa lugha. Huenda walifanya mambo haya yote, lakini hawakumjia yule Mtu, Kristo Yesu, na kwa kweli wakazaliwa mara ya pili. Moyoni mwao, vitu hivi hufa, asili hubadilishwa, na mtu mpya anazaliwa.

71 Sasa, Musa alipokuwa mtu mzima, alikataa kuitwa mwana wa binti Farao. Baada ya hayo akamwua yule Mmisri. Lakini Mungu alikuwa pamoja naye huko Midiani, kisha akamrudisha. Na mbele ya kile kichaka kilichowaka moto, siku ile, alipokea tukio ambalo lilidumu pamoja naye maadamu alikuwa yu hai. Na kama nilivyosema jana usiku, ndivyo ninasema leo, kwamba mtu. . .haidhuru Musa alifundishwa vizuri kiasi gani, alijua theolojia kiasi gani, jinsi alivyokuwa mshiriki mzuri wa kanisa. Pia alikuwa na mwalimu mzuri, mama. Alilelewa chini ya kila kanuni ya elimu ambayo ingeweza kuletwa. Alikuwa mwana wa mfalme. Lakini bado, akijaribu kwa nafsi yake mwenyewe, alishindwa kuvuka. Lakini katika dakika tano Mbele ya kichaka kilichowaka moto, akawa mtu mpya. Jambo fulani lilitukia.

72 Na kile tunachohitaji siku hizi, katika seminari zetu, sio kufundishwa theolojia nyingi sana, bali tukio la kichaka kinachowaka moto, ambapo watu hushuka mbele za Mungu na kukutana Naye uso kwa uso. Tunahitaji mpinzani siku hizi kama tulivyokuwa naye siku hiyo. Tunachohitaji ni wanaume na wanawake ambao wamekutana na Mungu, na wanajua kile wanachozungumzia. Sio mtu anayejaribu kufundisha kutoka katika kitabu fulani cha kanisa, au theolojia fulani iliyo wazi. Tunachohitaji siku hizi, ni mtu ambaye amekuwa mbele ya kichaka kinachowaka moto, amezaliwa mara ya pili, na kubadilishwa na kufanywa kiumbe kipya. Hiyo ndiyo aina ya mtu tunayemhitaji siku hizi. Huyo ndiye mtu ambaye atakaa kwenye mstari wa vita, bila kujali yajayo na yaendayo.

73 Musa, baada ya kupokea agizo lake, alishuka akaenda Misri na kuwakomboa wana wa Israeli. Kosa moja kubwa tunalofanya, na jambo moja kuu. Kama ilivyokuwa siku hiyo, ndivyo ilivyo siku hizi. Wakati, tunaona ya kwamba Musa alishuka na kuwachukua wana wa Israeli na kuwatoa, maajabu yalikuwa yamefanyika.

74 Sasa hili hapa. Sitaki kuwaudhi, sitaki kuwatikisa au kuwang'oa ngozi, lakini natamani kuhubiri Ukweli. Kuna jambo

moja juu yake, ndugu, Ukweli kamwe hautakufanya upendwe na watu, lakini Ukweli utakufanya kuwa mkweli. Hilo ni jambo moja zuri. Na si ni afadhali uwe mwaminifu kuliko kuwa maarufu? Bila shaka afadhali hivyo.

75 Sasa, nawatakeni mjue, ya kwamba, wakati maajabu hayo yalipofanywa, miujiza ilifanywa, ishara na maajabu. Na walipotoka, Biblia ilisema, "Umati wa watu waliochanganyikana ulitoka," umati wa watu waliochanganyikana. Baadhi yao, waaminio; wengine, wakijifanya wanaamini. Mi—miujiza mikuu ilikuwa imefanywa. Watu walitoka nje wakidai kuwa waaminio, wala hawakuwa waaminio.

76 Na hapo ndipo lundo kubwa la matatizo yetu lilipo siku hizi. Tunaweza kuweka kidole chetu juu yake. Ni wanaume na wanawake wanaokuja kanisani na kudai kuwa waaminio, wala si waaminio. Nimelipata mimbarini. Nimelipata kwenye mstari wa maombi. Nimelipata kila mahali, ambapo wanaume wanaingia, na wanawake, ambao walisema, "Mimi ni mwaminio," na kudai kuwa ni mwaminio, wala si waaminio.

77 Na hilo ndilo lililoanzisha matatizo ya Israeli. Walipofikia mahali, ambapo waliona watu hawa wametoka nje. Hakika, mambo ya kimbinguni yalikuwa yamefanywa.

78 Hilo ndilo tunalopata katika milki zetu siku hizi, katika makanisa yetu. Mungu amejitokeza jukwaani. Anaponya wagonjwa. Amewafufua wafu. Ameyafungua macho ya vipofu. Huwafanya viziwi kusikia, mabubu kunena. Anawaponya viwete. Anaondoa kansa kutoka kwa watu. Sisi . . . Hilo haliwezi kukanushwa. Hiyo ni kwa maelfu. Na wakati mmoja ilianza, kutoka papa hapa kwenye Barabara ya Nane na ya Penn, na sasa kote duniani pamoja na mioto elfu kumi ya uamsho inayowaka juu ya vilima vya kila taifa la makafiri na kwingine kote. Ishara na maajabu yanafanywa. Mambo makubwa yanaendelea. Mungu anatenda kazi! Tuko kwenye wakati wa mwisho, njia panda ya wakati.

79 Kwa hiyo tunaona, katika hili, unatokea umati wa watu waliochanganyikana. Mara nyingi, watu wa Mungu wakisema, "Naam, ndivyo nilivyo. Nitafanya *hivi*." Nasi tunaona ya kwamba watu hao walikuwa wa kimwili. Mara tu tatizo la kwanza lilipoinuka, wakatamani kurudi Misri. Walitaka vyungu vya vitunguu saumu. Walitaka samaki wa mtoni. Walitaka vitunguu na vitunguu saumu. Walitaka vitu walivyokuwa navyo huko Misri.

80 Huo ni mfano mzuri na mkamilifu wa mshiriki wa kimwili wa kanisa siku hizi. Anapenda mambo ya ulimwenguni kwa sababu yeye si wa Mungu. Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia au mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo

ndani yako." Na Kristo yuko sahihi katika matamshi Yake yote. Na hiyo ni kweli. Na siku hizi tunaona watu wakitoka nje . . .

81 Loo, laiti Mungu, kwa namna fulani, angaliweka hili upande wa kushoto, chini ya ubavu wa tano, na kulishindilia ndani. Mtu, haijalishi unajaribu kujifanya kiasi gani, tatizo likitokea, mtu ataonyesha uzuri wake na ubaya wake chini ya matatizo. Mchukue Mkristo wakati mwingine, na umweke chini ya matatizo uone jinsi anavyotenda, nawe unaweza kujua jinsi alivyoumbwa. Kila mtu anaweza kwenda vizuri, kila mtu anaweza kumsifu Bwana, wakati Roho Mtakatifu anashuka katika kusanyiko la watu; lakini hebu matatizo yazuke, uone yatakayotukia, angalia yatakayotukia basi. Kisha, unaanguka kote? Je, wewe ni mmoja wa umati wa watu waliochanganyikana? Wewe ni mtu ambaye huwezi, kama usemi wa mitaani unavyosema, "Huwezi kulimeza"? Hivyo ndivyo, huwezi kulistahimili. Ndugu, kama umeenda hivyo, kurudi nyuma na juu-chini, na kuingia-na-kutoka, mbona usije Kalvari na kujifia mwenyewe, na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu? Amina. Jioneeni aibu; ninyi mnaokiri Ukristo, ninyi mnaoishi makanisani mwenu.

82 Hatuna wafuasi hapa. Mnakuja tu hapa. Ninyi ni wa makanisa yote mbalimbali.

83 Lakini, ninyi watu mnaokiri kuwa Wakristo, halafu mnaishi kitu nje ambacho sivyo mlivyo, ninyi ni fedheha kwa jamii ya Bwana Yesu Kristo. Amina. Ninyi mnaokiri kuwa Wakristo, na mnaona haya kuliamini Neno Lake, au kushuhudia Nguvu na utukufu Wake, wakati wowote, wewe ni fedheha kwa Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina. Hiyo ni kweli. Hiyo ni sawa. Simama kwa Neno. Utumbukie au uzame, simama kwenye Neno Lake.

84 Ilimbidi Ibrahimu kufanya hivyo, na kuviita vitu ambavyo havikuwepo, kana kwamba vilikuwepo. Alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kuwa ana haki.

85 Tunachohitaji leo hii ni kuondolewa uti wa matamanio, ndipo uti wa mgongo uwekwe katika Ukristo. Upo. Kitu tunachohitaji ni baadhi ya Wakristo waliozaliwa mara ya pili, wanaume kwa wanawake, ambao, watakapoona shida ikitokea, hawataikimbia, hawataanguka, hawatakimbia *huku*, waishiriki, lakini mwanamume au mwanamke ambaye atasimama na kuonyesha rangi zao. Hata marafiki zako watakuthamini zaidi ikiwa utafanya hivyo.

86 Ni mwanamume gani, asiyemthamini mwanamke? Acha awe na sura mbaya kama uzio uliotengenezwa kwa udongo na kupakwa viluwiluwi. Acha awe na sura mbaya awezavyo kuwa, lakini hebu awe mama mwenye heshima katika tabia vya kutosha kuyasimamia maadili ya mwanamke. Hakuna mwanamume, nchini, ambaye hatamvulia kofia, kama ana wakia wa mume ndani yake.

87 Na kama mwanamume akikabiliana na hilo, akiwa mwana wa Mungu aliyeanguka, Mungu Mwenyewe atawazia nini juu ya mtu ambaye atasimama juu ya imani yake, kuita kweli "kweli," na uwongo "uwongo." Tunachohitaji leo hii ni uamsho mzuri, wa kale, wa Mtakatifu Paulo, na Roho Mtakatifu wa Biblia kurudi kanisani tena.

88 Kuna mengi sana ya huku kutokuwa na msimamo na kufanya yasiyofaa, kwa jina la Ukristo, kuondoa; umadhehebu mwingi, theolojia nyingi, elimu nyingi sana. Wala sijaribu kuunga mkono. . . Watu hawatembei, hata hivyo, vilema kadiri kanisa lilivyo. Hili hapa. Kadiri kanisa lilivyo kilema, elimu siyo gango lako. Imani yako ndiyo gango lako. Amina. Kweli. Elimu haitalifanikisha. Madhehebu hayatalifanikisha kamwe. Hakutawahi kuwa na shirika litakaloweza kuchukua nafasi ya lile tukio la chumba cha juu. Kamwe hakutakuwa na shule itakayochukua mahali pa Pentekoste. Haiwezekani. "Si kwa nguvu, wala kwa uwezo, bali kwa Roho Wangu, asema Bwana." Hilo ndilo tunalohitaji leo, kurudi kwenye ule ujuzi wa Biblia. Wakristo waliozaliwa mara ya pili, na wameoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo, wakafanywa weupe, kuzaliwa upya, waliozaliwa mara ya pili. Kile ulimwengu unachohitaji siku hizi: uamsho, uamsho wa mtindo wa kale, aina ile aliyokuwa nayo Mtakatifu Paulo yapata 66 A.D.

89 Sasa, ndugu yangu, dada, tunautazama umati huu wa watu waliochanganyikana ukipanda. Baada ya kitambo, wanaanza kulalamika.

90 Hilo ndilo tunalopata katika kila mwenendo wa Mungu. Hilo ndilo ninyi Methodisti mnaona katika kanisa lenu. Hilo ndilo ninyi Baptisti mnalopata katika kanisa lenu; ninyi Presbiteri, Wapentekoste, yeyote yule. Mnawapata. Ni umati wa watu waliochanganyikana. Ndivyo ilivyokuwa. Wakati John Wesley alipokuwa na uamsho, huko nyuma kabisa katika karne ya kumi na saba, umati wa watu waliochanganganyikana uliingia. Wakati Martin Luther alipokuwa na uamsho, umati wa watu waliochanganyikana ulipanda. Wakati Baptisti, wakiongozwa na John Smith, walipokuwa na uamsho, umati wa watu waliochanganyikana ulipanda. Wakati Pentekoste walipokuwa na uamsho, umati wa watu waliochanganyikana lilikwea. Na hilo ndilo hasa linaloliweka kwenye rafu. Kama ingalikuwa watu walio halisi kabisa, wangebakia kanisani, na wangewaombea hawa wengine watoke, na kuendelea. Bado kungekuwa na uamsho katika kanisa la Methodisti, Baptisti, Presbiteri, na la Kipentekoste. Ni umati wa watu waliochanganyikana.

91 Wakatoka. Mara tu walipofika kule, wakaanza kulalamika. Walikuwa tu wamekaa huko nje jangwani miezi mitatu, wakaanza kusema, "Loo, laiti ningalikuwa na kitunguu saumu! Laiti ningalikuwa na kitunguu!" Walikuwa huko

nje, nao walikuwa wamebadilisha chakula cha Malaika na kitunguu saumu, huku wakilalamika. Kwa nini? Matumbo yao hayakuweza kumeng'enya (kumudu) chakula cha Malaika.

92 Hiyo ndiyo shida siku hizi. Hatujawa na uamsho wa kale wa Roho Mtakatifu, nayo matumbo yetu ya kiroho hayawezi kumeng'enya uamsho halisi, mzuri, wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu, kushikilia uamsho. Vinginevyo; tunahitaji maagizo ya Daktari, hayo ni maagizo ya daktari Yesu, ambayo yatatuweka sawa. Bila shaka.

93 Hawashikilii. Wanaendelea; wanarudi nyuma. Kitu kidogo tu cha kwanza kinapotokea; wanalalamika, wanagombana, wanazozana. Wanachukua. . .Mojawapo ya mambo hayo linapoanza kanisani, ni kama kansa. Itaua kanisa zima. Hiyo ni kweli. Hilo linapoanza tunapaswa kuliondoa.

94 Sasa, wakati hawakuwa wamekwenda mbali sana. . . Sasa wazia, wakila chakula cha Malaika, kilichoshuka kutoka Mbinguni, nao walikuwa wakilalamika. Nao walikuwa wakinywa maji kutoka katika Mwamba uliopigwa; maji safi, matakatifu ya Uzima, nao walikuwa wakilalamika. Walitaka maji ya matope ya Nile.

95 Ndivyo ilivyo siku hizi! Watu wanasema, "Loo, mhubiri, wewe una akili finyu sana. Unaondoa raha zote kanisani, unapoanza kuhubiri dhidi ya mambo ya aina *hii* na mambo ya aina *ile*."

96 Ndugu, kama kanisa lingesimama mahali linapokiri, siku hizi, lingeyapenda mambo ya Mungu, na kuchukia mambo ya ulimwengu. Tuna umati wa watu waliochanganyikana, hiyo ndiyo shida siku hizi. Umati wa watu waliochanganyikana, watu wanaotamani mambo ya ulimwengu, nao wanataka kuendelea kucheza na kanisa. Huo ndio unaowafanya wajikwae na kuanguka. Huo ndio unaofunga mkutano wa maombi. Hivyo ndivyo, wamejipanga na kila namna ya vyama kanisani, na kuondoa madhabahu kwenye benchi ya mbele. Na moto pekee lililo nao ni kwenye orofa ya chini. Huo ndio unaomwambia mhubiri kuhubiri kwa dakika kumi na tano, na kuyafanya kwa rozari ama ndege wekundu, ama chochote kile.

97 Lakini, nawaambia, Kanisa lililozaliwa mara ya pili la Mungu aliye hai linataka kusikia Injili. Maana, mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, Yesu alisema ya kwamba . . . "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Hakika alisema.

98 Umati wa watu waliochanganyikana! Wakapanda juu. Naam. Walikuwa wameacha nyadhifa zao kuu za majivuno za Misri, wakijivunia mawazo yao ya mali, katika vifaa vyao vya mitambo, katika sayansi yao ya tiba, jinsi walivyokuwa katika mitambo yao. Walikuwa wakijivunia nyadhifa zao. Waliacha

hizo, wapate kusafiri na yule Tabibu mkuu, nao walikuwa wangali wanalalamika.

Je, hiyo si ni kama tu umati wa watu waliochanganganyikana siku hizi?

99 Na muda si muda mwajua, walifika mahali paitwapo Kadesh-barnea. Kadesh-barnea ndicho kiti cha hukumu, ilikuwa kiti cha hukumu cha ulimwengu. Jina halisi la mahali hapo, maana yake, ilikuwa, "chemchemi kubwa mno" iliyobubujika karibu na kundi hili la mitende lililosimama jangwani, ambapo baadhi ya vibanda vidogo, vilivyoitwa jiji, makao ya taifa la watu, au watu wachache. Na wakati wote pale, zile chemchemi ndogo sana zilizobubujika kila mahali, zilipata maji yake kutokana na chemchemi hii kubwa mno.

100 Ni picha nzuri jinsi gani ya kanisa, huko nje jangwani, ambapo kila kitu ilibidi kuja Kadeshi kupata maji. Ilibidi kila kitu kuja Kadeshi, kupata maji. Na kwa hiyo, hiyo chemchemi moja kubwa, ilichangia chemchemi hizo zingine. Huo ni mfano wa Mbinguni. Huo ni mfano wa kiti cha hukumu cha Mungu, ambapo hukumu inaanzia kwenye nyumba ya Mungu. Na pale ambapo chemchemi hii moja kuu ilimwagia, na chemchemi hizo zingine ndogondogo zikatoka kwake, maana yake, "Mbingu ikiwa ndiyo kiti cha hukumu cha Kristo, na makanisa yote yanatoa uzima, maji, katika kiti cha hukumu," popote pale watu wanapokuja kanisani kuhukumiwa.

101 Shida yake ni kwamba, siku hizi, watu huja kanisani nao wanapigwa-pigwa mgongoni, na kadhalika. Ni kwa sababu wanalipa kwenye sahani ya sadaka; kwa sababu wanakuwa shemasi; kwa sababu wanakuwa kitu kingine, cha kanisa. Au, ama, wanaweza kuendesha gari bora zaidi, au wanaweza kuvaa nguo nzuri zaidi, au—au kitu kama hicho. Unaheshimiwa na unapigwa-pigwa mgongoni.

102 Ndugu, tunachohitaji siku hizi ni wahubiri wa mtindo wa kale ambao wataita nyeusi "nyeusi," na nyeupe "nyeupe."

103 Kama vile Yohana Mbatizaji, alipotoka katika nyika ya Uyahudi, hakuwa amevalia vizuri sana. Alikuwa amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, na mshipi wa ngozi, amejizungushia kitambaa cha singa za ngamia. Naye akatoka akihubiri toba. Ndipo Herode alipomchukua mke wa Filipo ndugu yake, naye alikuwa amemwoa, akaja pale mkutanoni. Ninaweza kuwazia shemasi akisema, "Usihubiri juu ya ndoa na talaka usiku wa leo, kwa maana kuna mtu mashuhuri miongoni mwetu usiku wa leo. Usifanye kitu kama hicho."

104 Nanyi mwaweza kuwazia mtu aliyepokea Roho Mtakatifu katika tumbo la uzazi la mama yake, akiachilia kitu chochote ambacho ni dhambi? Yohana Mbatizaji alimpokea Roho Mtakatifu miezi mitatu kabla hajazaliwa. Alikuwa amekufa,

tumboni mwa mama yake. Jina la Yesu lilipotajwa kwa mara ya kwanza, aliruka-ruka ndani ya tumbo la mama yake. Je, unaweza kuwazia mtu aliyempokea Roho wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, miezi mitatu kabla hajazaliwa, akipatana na mambo ya dunia?

105 Akatoka moja kwa moja na kutia kidole chake chini ya pua yake, na kusema, "Si halali kwako kumchukua." Hiyo ndio njia. I—iligharimu kichwa chake. Lakini yeye ni asiyepatikana na mauti, usiku wa leo, miongoni mwa wale waliokombolewa, katika ulimwengu ule mwingine. Amina. Hilo halipendwi na watu, lakini ni Ukweli. Amina. Angalieni!

106 Msishtuke ninaposema, "amina." Inamaanisha, "Na iwe hivyo." Naam. Hiyo ni kweli. Sasa, najua mimi husisimkwa kidogo, mara moja moja. Mnafikiri nimesisimkwa, lakini sivyo. Najua mahali nilipo. Ninajua mahali nilipo hasa, najua ninachozungumzia. najua ninayezungumza habari Zake; Bwana Yesu Kristo. Angalieni jinsi linavyopendeza!

107 Nao wakaanza kunung'unika na kulalamika, ndipo hatimaye wakaletwa Kadeshi. Basi walipokuja Kadeshi, kiti hiki cha hukumu, hukumu, ndipo kitu hicho chote kikakusanywa pamoja.

108 Na siku moja tukufu, nami ninaamini siku hiyo imekaribia sasa hivi, wakati kutakuwa na utengano kati ya mema na mabaya. Na ninaamini ninaweza kuthibitisha vya kutosha, kwa mamlaka ya Kimaandiko, ya kwamba alama ya mnyama na Muhuri wa Mungu, ama watu wa Mungu, itatokea hivi karibuni, na hata sasa inatendeka. Alama ya mnyama ni alama ya ukengeufu. Alama ya mnyama ni wale walioikataa kweli; walitobolewa masikioni, wapate kuwa makosani siku zao zote. Wale wanaopokea Muhuri wa Mungu, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Waefeso 4:30 inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Imefika mahali ambapo mtu hawezi kusimama hivi hivi tena. Hiyo ni kweli.

109 Ni kama tu jamaa akijaribu kwenda Mbinguni. Alikuwa na tikiti kadhaa. Yule mtu akamuuliza wakati alipopanda treni, akasema, "Tiketi hizo nyingi ni za nini?" Moja yazo ilikuwa ni ya Methodisti, moja ya Baptisti, moja ya Sayansi ya Kikristo, moja ya Adventista ya Sabato, moja ilikuwa ya kila kitu. Kasema, "Umenunua tiketi hizi zote za nini?"

110 Akasema, "Vema, nitakwambia, bwana." Kasema, "Mmoja aliendelea kusema *hili* lilikuwa ni la kweli, na *lile* ni la kweli, ndipo nikayajaribu yote." Kasema, "Nilifikiri nilete tiketi kutoka kwa kila moja yao." Naye akatiwa hatiani.

111 Ndugu, kuna njia moja tu ya kufika Mbinguni, hiyo ni kupitia Kristo Yesu, kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu.

"Mtu asipozaliwa mara ya pili, hataingia ule Ufalme," alisema Bwana wetu Yesu Kristo. Amina.

112 Ni siku ya jinsi gani tunayoishi, ewe rafiki! Ni wakati wa jinsi gani tunaoishi! Ni badiliko la jinsi gani! Ni mtikiso wa jinsi gani! Mungu daima amelithibitisha Kanisa Lake. Mungu atafanya hivyo, daima! Sisemi wote waje kwenye Maskani ya Branham. Sitasema wote waende Wall Street. Sisemi wote waende kwenye kanisa la Kikristo, ama kanisa lolote lile. Ninasema ya kwamba Mungu, katika kila kanisa, anao washiriki Wake, anao washiriki Wake wa Mwili Wake ambao wamezaliwa mara ya pili. Na hao ndio walio wakweli kwa Mungu. Hao ndio wanaompenda Bwana Yesu kwa moyo wao wote, na kwa nafsi yao yote. Utawakuta wakisoma Biblia yao, katika mkutano wa maombi, wakifanya kila wawezalo kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Hiyo ni kweli.

113 Lakini umati wa watu waliochanganyikana una nguvu mno, hata kupita kiasi, nao wanajaribu kuwavuta nyuma kuwaingiza katika mambo ya ulimwengu. Tunachopaswa kuwa nacho siku hizi ni Kadesh-barnea nyingine, hiyo ni kweli, ambapo hukumu huanzia.

114 Basi ilikuwaje? Kora alisimama na kusema, "Kuna watu wengi zaidi watakatifu mbali na Musa." Naye akakusanya kundi kubwa pamoja. Ndipo anatoka basi pamoja na kundi hili kubwa, na kusema, "Sisi ni manabii. Nasi ni *hiki*, nasi ni *kile*."

115 Basi ilikuwaje? Mungu akamwambia Musa, akasema, "Jitenge naye." Ndipo akaifungua ardhi na kuwameza. Huo ndio ulikuwa mwisho wa wanung'unikaji hao, na mwisho wa wale watu walioambatana na Kora.

116 Basi nini kilitokea? Mungu akasema, "Tutaninii. . ." Akamwambia Musa, "Watume baadhi ya wapelelezi wakaipeleleze nchi tunayokwenda, ambako nimewaahidi." Iwapo Mungu aliwaambia ilikuwa ni nchi nzuri, kama Mungu alitoa ahadi Zake zote, hilo lilionekana kana kwamba linapaswa kumridhisha mtu yeyote, kama Mungu alisema hivyo.

117 Sasa, tuta—tutapiga kelele, kila wakati, "Bwana asifiwe," kwa hilo. Lakini, ndugu, Mungu yeye yule aliyewatolea ahadi hiyo anatutolea kila ahadi aliyowapa. Kwa nini tuishuku?

118 "Unajaribu kusema nini, Ndugu Branham? Je, ni umati wa watu waliochanganyikana?" Naam, hasa, hiyo ni kweli. Ni umati wa watu waliochanganyikana. Nasi tuko Kadeshi sasa hivi, ambako mtaninii. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

119 Watu mashuhuri nchini! Tumekuwa na Jack Schuler, Billy Graham. Tumekuwa na Oral Roberts, Tommy Hicks, Tommy Osborn. Tumekuwa na watu wengi hodari walioenda huku na huko kote katika taifa hili. Na, usiku wa leo, kuna vilabu vingi vya kuuza pombe haramu kuliko makanisa. Na

vinaendelea kupanuka. Kuna nini? Kuna umati wa watu waliochanganyikana.

120 Hebu niwaambieni jambo fulani. Hebu taifa hili si kwamba tu liagize saa moja, siku fulani, iliyotengwa kwa ajili ya mkutano wa maombi, ambapo takriban asilimia moja ya elfu moja watajaribu kuhudhuria. Hebu taifa hili zima limgeukie Mungu, na kubomoa kila kilabu cha pombe haramu, libomoe kila kiwanda cha pombe, na kubomoa kila mahali pa kunywea pombe, na vitu vyote; na kuwavua wanawake maskini kaptura hizi chafu, na kuifanya kuwa hatia ya kifungoni kuzivalia barabarani; na kuyasafisha makazi, na nyumba, na kanisa; na kuwaweka wahubiri nyuma ya mimbara, badala ya namna fulani ya watoa hotuba; kusababisha uamsho wa mtindo wa kale, ambapo wanaume na wanawake watamlilia Mungu, tutakuwa na uamsho ambao utaenea nchini, na ndio ulinzi bora zaidi ambao tumewahi kuwa nao. Ndicho kitu pekee ulimwenguni kitakacholizuia bomu la atomiki. Una kimbilio la bomu, chini ya ubawa Wake. Amina. Hiyo ni kweli. Angalieni.

121 Kadesh-barnea ilifikia mahali ambapo ilibidi kuwe na hukumu. Ndipo Musa akawachagua kumi na wawili, mmoja kutoka katika kila kabila, kisha akawatuma waende kuipeleleza nchi.

122 Waliporudi, laiti mngaliona ni taarifa ya jinsi gani! "Loo," wakasema, "ni nchi nzuri. Loo, ni nchi ya ajabu. Imejaa maziwa na asali."

123 "Lakini," kumi kati yao wakasema, "hatuwezi kuiteka. Hatuwezi. Loo," kasema, "tulikutana na Wa—Waamori, Wamidiani, na—na Wakanaani, na wote hao. Mbona, tulionekana kama panzi, kando yao. Hao ni jamaa wakubwa mno. Nayo miji yao yote imezingirwa na kuta, wala kamwe hakuna njia ya sisi kuingia ndani. Loo, mioyo yetu inazimia ndani yetu. Hatuwezi kuichukua." Na, kura ya maoni ya watu wengi, watu wakaipokea.

124 Lakini hapo walisimama watu wawili, mmoja jina lake Kalebu, na mmoja jina lake Yoshua, ambao walileta kichala cha zabibu, kilichowalazimu watu wawili kukibeba. Kalebu akasema, "Tulieni, mbele ya yule nabii. Tulieni." Akasema, "Tuna uwezo wa kuiteka. Hima twendeni tukaitamalaki, mara moja!"

125 Tunachohitaji katika majira haya ni mtu wa kuisahi ahadi ya Mungu mbele ya watu. Mungu aliahidi kumwagwa kwa baraka za kipentekoste katika siku za mwisho, ninamaanisha kumwagwa halisi kwa kipentekoste, na wakati wa kuja kwake umewadia. Kadesh-barnea nyingine imefika. Naam, bwana.

126 Walisema, "Tunaweza kabisa kufanya hivyo. Hakika, tunaweza kufanya hivyo." Ilikuwa ni nini? Hao wafuasi waoga wa kanisa walikuwa wakiangalia kile walichoweza kuona kwa

macho yao, lakini Kalebu na Yoshua walikuwa wakiangalia ahadi ya Mungu. Sijali walikuwa na upinzani kiasi gani, jinsi hao majitu walivyoonekana wakubwa, jinsi nyua zilivyoonekana kubwa, walikuwa wanaangalia ahadi ya Mungu.

127 Na kila mwanamume na mwanamke usiku wa leo, anayetaka kuendelea pamoja na Mungu, hazingatii yale ulimwengu usemayo, kama tunaweza au hatuwezi; Mungu aliliahidi, na hilo latosha. "Mungu alisema hivyo!" Nalipenda hilo. Mungu anaposema hivyo, hilo latosha milele.

128 Nawaambia, usiku wa leo. Tumekuwa na kujifanya kwingi kwa uwongo. Tumekuwa na imani nyingi za kujibunia. Tumekuwa na upuuzi mwingi ambao ulifanywa kwa maonyesho. Bila shaka. Ibilisi daima hukutupia watangulizi wake, kama kitu cha bandia apate kuwatisha watu. Tumekuwa na Pentekoste ya uwongo. Tumekuwa na mvua ya uwongo. Tumekuwa na *hiki* na *kile* cha uwongo.

129 Lakini katikati ya kila sehemu yake, kuna ubatizo halisi wa Roho Mtakatifu. Kuna baraka halisi ya kipentekoste, tena. Kuna uponyaji halisi wa Kiungu. Kuna Roho wa kweli. Kuna watu wa kweli. Na wakati wa maandamano umewadia. Hiyo ni kweli.

130 Watu, kwenye saa ya uamuzi sasa! Inakubidi kufanya uamuzi. Kanisa hili halina budi kufanya uamuzi. Kila mtu hufikia mahali ambapo kuna saa muhimu sana. Kulikuwa na wakati muhimu uliofika ambapo ilibidi ujiamulie. Kiti cha hukumu, ulikuwa humo. Ilikubidi kusema, "Nina hatia," au, "Sina hatia." Unaposimama mbele ya hakimu, huna budi kujiamulia.

131 Na, usiku wa leo, Maskani ya Branham haina budi kujiamulia. Ama tutaendelea mbele au turudi nyuma. Hiyo ni kweli. Mnarudi kwenye vitunguu saumu na—na vitunguu, na upuuzi wa Misri, ama mnasonga mbele kwenye chakula cha Malaika, kwenye nchi ya ahadi ambapo Mungu alitoa ahadi. Tunakwenda kwenye uamsho wa mtindo wa kale, wa Roho Mtakatifu; au utakaa bila msimamo, ukitangatanga huku na huko, na kudonoa kama robini kwenye tofaa, hadi siku utakapokufa. Huna budi kufanya uamuzi. Huwezi kuendelea. "Kwa nini kusitasita kati ya mawazo mawili?" akasema Eliya. "Mungu akiwa ndiye Mungu, mtumikieni. Ikiwa Yeye si Mungu, basi msimtumikie."

132 Ikiwa ujuzi halisi wa Mungu ndio unaoondoa dhambi kutoka kwa moyo wa mwanadamu, wala si kuwa mfuasi wa kanisa, au kuwa wa ukoo fulani, au kuwa wa shirika fulani, ambalo sina la kusema dhidi yake. Vitu hivyo ni sawa. Kama . . .

133 Elimu haitalileta. Tumejaribu mara nyingi tukapata mabirika yavujayo kutoka kwake. Tulifikiri, wakati mmoja, tulipokuwa na wale Mabingwa Wanne, kwamba wangetatua vita vyote. Haikutatua vita. Ilikuwa inavuja. Tulifikiri, wakati

mmoja, kwamba mfumo wa elimu ungeokoa ulimwengu mzima. Nasi tukaelimisha, na tumepata nini? Kundi la makafiri wenye elimu. Hiyo ni kweli kabisa. Tulifikiri kwamba mashirika yangeuokoa ulimwengu. Nasi tumegundua kuwa wahalifu walio wabaya zaidi tulio nao wanatoka katika yanayoitwa mashirika yao. Elimu na shirika hazitauokoa ulimwengu.

134 Kuna Mwokozi mmoja tu kwa ulimwengu, na huyo ni Damu ya Yesu Kristo ambayo ilimwagwa bure pale Kalvari, kwa ajili ya ondoleo la kila dhambi ambayo mwanadamu aliwahi kutenda. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya ninii Yake. . . amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Ninampa changamoto mwanamume au mwanamke yeyote, katika Jina la Yesu Kristo, kuiamini ahadi ya Mungu, usiku wa leo, aone kama ni ya kweli ama ni ya uongo.

135 Nimewaona wafu wakifufuliwa; wakati madaktari walipoondoka, wakisema wamekufa. Nimeona vipofu wakifanywa kuona, walikuwa vipofu kabisa kwa miaka na miaka. Nimewaona viziwi, na vipofu, na vilema, na viwete; wakichupa, na kuruka, na kumsifu Bwana. Nimewaona makahaba wakitoka mtaani na wakawa wanawake wenye heshima. Nimeona walevi wakitoka kwenye bwalo la kucheza kamari, na mahali pa hila za ulimwengu huu, na wakawa waungwana na watakatifu. Ninampa changamoto mtu yeyote atoe kitu kingine ambacho kitafanya hivyo.

136 Nimeona mtu ambaye alichukua Shirika la Kuwasaidia Walevi Sugu na kujaribu kutibiwa. Akadungwa sindano, akanywa kila kitu, na saikolojia yote ulimwenguni, na aina bora zaidi ya madaktari ambao wangeweza kupatikana kuwapa matibabu, nao wakashindwa. Kisha nimemwona mtu yuyo huyo akiinuliwa na Damu ya Yesu Kristo, na kufanywa mtakatifu wa Mungu, na mhubiri wa Injili. Amina.

137 Mnafikiri mimi ni mtakatifu anayejibingirisha? Labda ndivyo nilivyo. Kweli! Lakini ikiwa inahitaji jina la "mtakatifu anayejibingirisha" kupata kibali kwa Kristo, na kuhukumiwa na ulimwengu, basi mimi ni mmoja wao. Hiyo ni kweli. Angalieni. Nampenda.

138 Una uamuzi wa kufanya. Uko Kadeshi, unaona; unaona, huwezi kusimama muda mrefu zaidi. Kwa nini unasitasita kati ya maoni mawili? Kwa nini kanisa haliwaki moto? Kwa nini mahali hapa hapajajaa watu? Kwa nini ishara kuu na maajabu makubwa hayafanyiki? Usimwekelee mchungaji. Ni wewe. Tuna umati uliochanganyikana; mmoja akivuta upande mmoja, na mwingine upande mwingine. Inakubidi ufikie wakati wa uamuzi. Ikiwa ni mchungaji, mwondoeni, mwondoeni na mweke mtu mwingine ambaye atachukua mahali pake. Kama ni shemasi, mwondoeni katika halmashauri na kumweka

mtu mwingine mahali pake, atakayepachukua mahali hapo. Utafanya nini, ndugu? Mungu ameweka jukumu hilo juu yako. Ndivyo ilivyo. Nasi, kila mmoja, hatuna budi kuwajibikia dhambi zetu wenyewe, na kujibu kwenye Siku ya Hukumu. Tuko Kadesh-barnea!

139 Nalo Neno la Mungu lilisema tunaweza kuiteka. Neno la Mungu lilisema tunaweza kuwa na uamsho. Neno la Mungu lilisema ya kwamba Yeye angeinua katika siku za mwisho, ishara na maajabu haya yote. Naye amefanya hivyo. Kila mtu anasimama mahali pake, lakini jambo litupasalo kufanya ni kukusanyika pamoja na kuanzisha uamsho. Tunaweza kufanya nini? Huenda uamuzi wako ukaja sasa. Uamuzi wako unaweza ukaja wakati mwingine. Lakini kama umekuja sasa, afadhali uuitikie. Unasema, "Loo, ndugu, mimi . . . Vema, nitafanya uamuzi siku moja." Huna budi kuufanya. Na sasa hivi ndio wakati wa kuufanya. Kuna wakati ambapo ilikubidi . . .

140 Ulipokuwa ukichumbiana na mkeo, ndugu yangu, ilikubidi kuamua ikiwa mtaoana au la. Ilikubidi kuamua. Inaweza kutokea, wengine wakisema hivi, "Hupaswi kuoa." Wengine wanasema, "Naam, afadhali uoe." Mmoja anasema, "Vema, una furaha zaidi ikiwa umeoa." Mwingine anasema, "Unakata koo lako." Mambo haya yote mbalimbali. Ilibidi uamue. Hiyo ni kweli. Hukumu, za Kadesh-barnea, zinakujia.

141 "Labda baadhi yenu hapa mnapaswa tu kupewa talaka." Inabidi kuwe na wakati, wakati fulani, ambapo tofauti zinakuja katika familia. Hazina budi kutatuliwa, kwa namna fulani. Inakubidi kuamua. Hebu nikwambie, ndugu yangu, usiku wa leo, uamuzi wa kufanya, ni, wewe na mkeo mkumbatiane, kama mtainama mbele za Mungu, na kupiga magoti, na kuamua ya kwamba mtamtumikia Yesu Kristo, na Yeye pekee, ndipo mahakama za talaka zitakauka. Kweli! Hakuna haja ya kuzungumza na wakili wako. Mazungumzo na Mwokozi wako yanahitajika. Hiyo ni kweli. Wakili anaweza kukupa ushauri, lakini Mwokozi anaweza kukuokoa. Wakili anaweza kukupa saikolojia, baadhi ya masomo yake ya kiakili, lakini Yesu Kristo anaweza kukupa neema na upendo Wake. Utachukua mahali pa hayo yote.

142 Ikiwa wewe ni mgonjwa usiku wa leo, inakubidi kufanya uamuzi, kama utamkubali Kristo kama mponyaji wako, au la. Huwezi kuwa bila msimamo, kusitasita nao. Unapaswa kusema, "Ninamwamini," au, "Simwamini." "Nitakuwa mzima," au, "siwezi. Sina imani ya kutosha kuwa mzima." Huna budi kufanya uamuzi wako.

143 Kama wewe ni mwenye dhambi, usiku wa leo, huna budi kufanya uamuzi. Uko Kadesh-barnea. Uko mahali pa kiti cha hukumu.

144 Chemchemi hizo ndogo zilikuwa nini? Ni makanisa, yanayowakilisha, yaliyotoka, ambapo hukumu inaanzia kwenye nyumba ya Mungu. Yesu alisema hivyo. Bi—Biblia ilisema hivyo. Hukumu huanza katika nyumba ya Mungu. Tuko katika nyumba ya Mungu, usiku wa leo, nawe huna budi kufanya uamuzi wako.

145 Huna budi kufanya uamuzi wako, kama utamjia Kristo, ama kama utamkataa usiku wa leo. Kila mwenye dhambi hapa ndani hana budi kufanya uamuzi huo sasa hivi.

146 Ama utatoka nje ya mlango huo, mwanamume au mwanamke bora kuliko vile ulivyoingia, au utatoka mbaya zaidi kuliko ulivyokuwa wakati ulipoingia. Huwezi kusimama vivi hivi usiku wa leo. Huna budi kuamua.

147 Hili lilikuwa moyoni mwangu, sasa liko . . . Lilikuwa moyoni mwangu, sasa liko mkononi mwako. Huna budi kufanya uamuzi wako. Na inakubidi kuamua. Labda umekuwa mshiriki mzuri wa kanisa. Labda sikuzote umekuwa na shauku kwamba ulimtaka Mungu zaidi. Huenda ulitaka kumfanyia Mungu jambo fulani. Kumbuka, wewe ni mwanadamu mara moja tu, na huo wakati mmoja ndio wakati pekee ambao utakuwa mwanadamu. Na huu unaweza kuwa ndio wakati ambao unapaswa kufanya uamuzi wako. Ama utasonga mbele pamoja na Mungu, ama ubaki mahali ulipo.

148 Huenda ukalazimika kufanya uamuzi wako usiku wa leo. Ikiwa ndivyo, naomba kwamba utatupilia mbali kila kitu. Kumbuka, sijali ni nini, ikiwa ni kazi, ikiwa ni familia, ikiwa ni wapendwa, ikiwa ni washirika, ikiwa ni wenzako, au yeyote yule, achilia kila kitu. "Atiaye mkono wake kwenye jembe la kulima, na hata akageuka kuangalia nyuma, hafai kulima." Hiyo ni kweli. "Weka kando kila mzigo mzito na dhambi ikuzingayo kwa urahisi." Hiyo ni nini? "Wekeni kando kila mzigo mzito, na kutokuamini kuwazingao kwa urahisi, na kukimbia mbio hizi kwa saburi, zilizowekwa mbele yenu."

Na tuombe.

149 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninaumalizia ujumbe huu mdogo, na kuutupa juu ya mioyo ya watu. Wewe ujuaye moyo wa wanaume na wanawake wote, Wewe ujuaye moyo wa kila mvulana na msichana, unajua moyo wa kila mtu. Unaujua moyo wangu. Na kote kote kutoka mimbarani hadi kwa bawabu, Bwana, Wewe wajua moyo wa kila mtu. Unajua tunachohitaji. Hatujui sisi. Jambo moja tu tujualo, tunajua tunamhitaji Yesu.

150 Na, Ee Kristo wa Mungu, unaweza kuahidi (la, Bwana) na usitimize? Ulisema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao. Na kama wakiomba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Ni changamoto iliyoje kwa kanisa letu, Bwana! Ni changamoto iliyoje kwa jamii

yetu! Ni changamoto iliyoje kwa watu wetu, usiku wa leo, uliyotupa Wewe! "Ukipungukiwa na chochote, mwombe Mungu. Atakupa."

151 Sasa ninaomba, Baba Mpendwa wa Mbinguni, kwamba, usiku wa leo, kwamba utamwaga Roho Mtakatifu bure, wa kusadikisha, na kusadikisha kila moyo kuhusu hitaji lao. Na langu, pamoja nalo, Bwana, tunapokungojea Wewe, katika Jina la Kristo.

152 Sasa huku tumeinamisha vichwa vyetu, huyo dada atatupa sauti kwenye kinanda. Nitawaulizeni swali. Huenda huu ukawa ndio wakati wako wa kufanya uamuzi.

153 Ni wangapi hapa ndani, kuna mwanamume mmoja ama mwanamke, mvulana au msichana, ambaye si Mkristo, ambaye ni mwenye dhambi? Nawe unataka kufanya uamuzi kwa ajili ya Yesu Kristo, na unahisi ya kwamba kitu Fulani kinabisha moyoni mwako wakati huu? Je, utainua mkono wako kwa uamuzi wako, na kusema, "Sasa ninafanya uamuzi wangu wa kumtumikia Kristo"? Mungu akubariki, bwana. Mtu mwingine? "Sasa ninafanya uamuzi wangu." Mungu akubariki, ewe msichana. Mtu mwingine? Mungu akubariki, hapo nyuma, ewe msichana.

154 Mtu mwingine, ufanye uamuzi wako? "Sasa nitamtumikia Kristo. Nimefika mwisho. Nimefika kwenye matatizo. Hii ndiyo saa. Niko Kadesh-barnea. Mungu amesimama moyoni mwangu. Je, ninaweza kuvuka? Je, ninaweza kumwacha rafiki yangu? Je, ninaweza kumwacha mshirika wangu wa duniani? Je, ninaweza kuvuka mpaka kule, kuingia katika nchi ya ahadi ambako Mungu aliahidi? Je, nitakuwa Kalebu, nitakuwa Yoshua, katika historia ya wakati. Je, nitakuwa Kalebu au Yoshua katika vitabu vya Mungu? Au, je, usiku wa leo, nitarudi nyuma na tabia yangu ya woga, ya manjano, na kurudi nyuma?" Mungu, ondoa hilo kutoka kwa kila mwanamume na mwanamke, na uwafanyie uamuzi, mfanyie Kristo usiku wa leo. Je, utainua mkono wako? Mimi . . . Mmoja zaidi. Mungu akubariki. Nakuona huko nyuma.

155 Mtu mwingine? Huko nje, waweza kutembea hadi dirishani mahali fulani? Na kuweka mkono wako juu ya dirisha, ukisema, "Nitafanya uamuzi wangu kwa ajili ya Kristo. Niko Kadesh-barnea, Ndugu Branham."

156 Je, kuna mtu mwingine humu ndani ambaye angefanya hivyo? Kuna aliyerudi nyuma angesema, "Nitafanya uamuzi wangu, usiku wa leo. Njia za mvunja sheria ni ngumu. Sitautumikia tena ulimwengu. Tangu usiku huu, na kuendelea, nitamtumikia Kristo. Sasa ninafanya uamuzi wangu. Nitainua mkono wangu. Nimekuwa mwenye dhambi. Nami nimekuwa Mkristo, lakini nimerudi nyuma, nami ninataka Mungu anirehemu."

157 Je, kuna mmoja hapa usiku wa leo, ambaye ni Mkristo, ambaye ni mwanaume au mtu wa Mungu, lakini umekuwa mvivu njiani, hujafanya vile Mungu alivyokwambia. Umekuwa huku na huko. Umesikiliza mambo ambayo hukupaswa kusikiliza. Umefanya mambo ambayo hukupaswa kufanya, nawe unataka Mungu akusamehe. Na unataka mwanzo mpya tangu usiku wa leo na kuendelea. Utafanya uamuzi wako kwa ajili ya Mungu sasa hivi, na kusema, "nitafanya hivyo"? Je, utainua mkono wako? Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Loo, hiyo ni sawa. Vema.

158 Kuna mtu mwingine yeyote utakayeinua mkono wako? Nataka uinue mkono wako. Huo ni msimamo wako, kwa Mungu. Mungu anauona mkono wako. Unasema, "Hilo lina manufaa gani?" Loo, inua mkono wako wa kuume wakati mmoja, kwa Mungu, uone unavyofanya. Inua mkono wako wa kulia, mahakamani, uape uwongo, ndipo uone kitakachokupata, utakamatwa nacho. Inua mkono wako kwa Mungu na ule kiapo, uone kama Roho Mtakatifu hakukamati kwake. Mungu anapokuwa kwenye mlango wa moyo wako, unafanya uamuzi wako.

159 Uko Kadesh-barnea. Huko ng'ambo ndiko kuna kila baraka ambayo Mungu alikuahidi. Huko kuna uamsho wa mtindo wa kale. Huko kuna furaha, amani, uvumilivu, fadhili, utu wema, upole, saburi, vimewekwa mbele yako, nawe hunayo. Ni yako. Mungu amekuahidi. Je, unaitaka?

160 Je, kuna familia hapa, inayokaribia kuvunjika? Mnabishana na kugombana ninyi kwa ninyi, na mnajua hampaswi kufanya hivyo. Unaaibika, jinsi unavyotenda karibu na mkeo, au mumeo, nawe unamtaka Mungu, usiku wa leo, kwa neema Yake, akupe neema ya kushinda, kumkumbatia kwa mkono wako, na kusema, "Mpenzi, kwa neema ya Mungu, kuanzia usiku wa leo na kuendelea, uamuzi wetu, 'Nitamwishia Mungu.'" Inua mkono wako. Je, kuna familia? Kila mtu ukiwa umeinamisha kichwa chako sasa. Inua tu mkono wako. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ninashukuru sana kwamba hakuna. Lakini kama ipo, Mungu anajua jinsi ya kushughulikia mambo yote.

161 Je, kuna mtu hapa usiku wa leo ambaye amekuwa mgonjwa, kwa muda mrefu? Na labda, unaonekana kana kwamba umeombewa, lakini huna imani ya kushinda. Lakini sasa hivi, kwamba utafanya uamuzi wako. "Bwana Mungu, tangu saa ii hii, nitakutumikia Wewe. Nami ninatoka hapa, nikishuhudia neema ya Mungu, ya kwamba kwa kupigwa Kwake nimeponywa. Nami nitaamini hilo, tangu usiku huu na kuendelea." Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki wewe, na wewe. Ajabu. Hiyo ni kweli. Nitawaombea baada ya dakika chache. Nitamwomba Mungu akujalie.

162 Sijui, usiku wa leo, kama mmoja wa watu ambaye si Mkristo,

angependa kutembea hadi madhabahuni na kupiga magoti? Madhabahu iko wazi. Ikiwa ungependa kuomba maombi ya wazi kwa Mungu, madhabahu iko wazi. Kwa mtu aliyerudi nyuma au kwa msafiri, yeyote yule, madhabahu iko wazi. Umekaribishwa. Uko Kadeshi. Hukumu inaendelea. Mungu amesimama akiwa amenyoosha mikono, tayari.

163 Yule mgonjwa angetaka kusimama kwa miguu yake, afanye maungamo ya hadharani kwamba sasa wamemkubali Kristo kama Mponyaji wao. Na kusema, "Tangu usiku huu na kuendelea, nitamwamini Mungu," na waombewe dua. Ikiwa ungependa, unakaribishwa kusimama kwa miguu yako. Vema.

Watatu kati yenu wamesimama. Endeleeni tu kusimama, mkipenda.

164 Sasa, Baba wa Mbinguni, wakati wakiwa wamesimama kwa miguu yao, Roho Mtakatifu amekuwa akizungumza. Nami nakuomba Wewe, Baba wa Mbinguni, kwamba mtu huyu atajaliwa rehema Zako, wote wawili, na mwanamke huyu, na mwanamume huyu mwingine aliyesimama hivi punde. Ee Mungu wa Milele, kwa kupigwa kwa Bwana Yesu Kristo, waliponywa. Mungu, umeishusha. Umeifanya halisi kwa watu. Nami naomba... Bwana, Wewe ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu." Na sasa Roho Mtakatifu amezungumza nao, na hakuna kitu kingine kinachoweza kufanywa. Wamefanya uamuzi wao, ya kwamba usiku wa leo wanakukubali Wewe kama mponyaji wao. Nao wanatoka kwenye maskani hii wakiamini ya kwamba watapona na kuwa wazima.

165 Bwana, haiwezi kushindwa, si zaidi ya vile Mungu awezavyo kushindwa. Tunatambua kwamba hakuna mtu aliye zaidi ya neno lake. Na usiku wa leo, wanaamini na wamekubali. Nao wataipokea, Bwana, ninapowaombea maombi haya ya imani, katika Jina la Kristo. Amina.

166 Mwaweza kuketi. Mungu awabariki. Amini hilo kwa moyo wako wote, shida zako zimekwisha.

167 Ni wangapi wanaompenda na wangetaka kwenda Sayuni pamoja Naye? Hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa. Hilo ni zuri sana. Haijalishi wewe ni wa kanisa gani. Vema.

168 Hebu na tusimame kwa miguu yetu sasa tunapoimba *Peleka Jina La Yesu.* Vema, dada, kama utatupa...

> ...Jina la Yesu...

169 Sasa geuka moja kwa moja na kupeana mikono na mtu aliye karibu nawe. Fikia pande zote na upeane mikono.

> ...ya ole;
> Litakupa furaha na faraja,
> Peleka kila uendako.

Loo Jina la thamani, (Jina la Thamani!) Lo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) Lo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

170 Wote wampendao, mno, kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, kwa nia yako yote, kwa nguvu zako zote, inua mkono wako *hivi,* na useme, "Bwana asifiwe." [Kusanyiko linasema, "Bwana asifiwe."—Mh.] Hilo ni jema. Vema, sasa:

Tukiliinamia Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Mfalme wa wafalme. . .
Safari yetu itakapokamilika.

Jina la thamani, Lo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Lo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la dunani na furaha ya Mbinguni.

56-0527 Huko Kadesh Barnea
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org